

‘Aqiydah Ahl-is-Sunnah wal-Jamaa’ah
Imaam Muhammad bin Swaalih bin ‘Uthaymiyn

‘Aqiydah Ahl-is-Sunnah wal-Jamaa’ah


Mwandishi:

Imaam Muhammad bin Swaalih bin ‘Uthaymiyn

Tarjama:

Firqatunnajia.com

Utangulizi	5
‘Aqiydah yetu	7
Kumuamini Allaah.....	22
Kuwaamini Malaika.....	24
Kuamini Vitabu	27
Kuamini Mitume	31
Kuamini siku ya Qiyaamah	39
Kuamini Qadar	46
Matunda ya ‘Aqiydah hii.....	53



Himdi zote anastahiki Allaah Pekee. Swalah na salaam ziwe juu ya yule ambaye hakuna Nabii mwingine baada yake, kizazi chake na Maswahabah zake.

Amma ba’d:

Nimepitia ‘Aqiydah ilio nzuri na yenyewe kutosheleza ambayo imeandika ndugu yetu ‘Allaamah muheshimiwa Shaykh Muhammad bin Swaalih bin ‘Uthaymiyn. Nimeisikia yote na kuona kuwa imebainisha ‘Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa’ah katika mlango wa Tawhiyd ya Allaah na Majina na Sifa Zake, katika mlango wa imani ya kuwaamini Malaika, Vitabu, Mitume, siku ya Mwisho na Qadar; kheri na shari yake.

Amefanya vizuri kuikusanya na amenufaisha. Humo ametaja yale anayoyahitajia mwanafunzi na kila muislamu katika imani yake ya kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Wake, Mitume Wake, siku ya Mwisho na Qadar; kheri na shari. Ameongezea juu ya hayo faida zinazohusiana na ‘Aqiydah ambazo huenda zisipatikane katika vitabu vingi vilivyoandika kuhusiana na ‘Aqiydah.

Allaah amjaze kheri na amzidishie elimu na uongofu. Allaah anufaishe kupitia kitabu chake hichi na vitabu vyake vingine vyote. Allaah atujaalie sisi, yeye na ndugu zetu wengine wote tuwe katika waongofu wenye kuongoza wanaolingania katika dini ya Allaah kwa ujuzi. Hakika Yeye ni Msikivu, yukaribu.

Swalah na salaam zimwendee Mtume wetu Muhammad, kizazi chake na Maswahabah zake.

Imeandikwa na kiumbe fakiri wa Allaah:

‘Abdul-‘Aziyz bin ‘Abdillaah bin Baaz - Allaah amsamehe - ambaye ni Muftiy
wa Saudi Arabia.

Utangulizi

Himdi zote anastahiki Allaah, Mola wa walimwengu. Mwisho mwema ni wa wachaji Allaah na uadui ni kwa madhalimu. Ninashuhudia ya kwamba hakuna mungu mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allaah, hali ya kuwa peke yake hana mshirika, Yeye ndiye Mfalme na haki iliyo wazi, na ninashuhudia ya kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake, ambaye ndiye Mtume wa mwisho na kiongozi wa wachaji Allaah. Swalah na salaam zimwendee yeye, ahli zake, Maswahabah zake na wale wenye kuwafuata kwa wema mpaka siku ya Qiyaamah.

Amma ba’d:

Hakika Allaah (Ta’ala) amemtuma Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) kwa uongofu na dini ya haki ili awe ni rahmah kwa walimwengu, kiigiezo kwa watendaji na hoja kwa viumbwe wote.

Kupitia kwake na Kitabu na Hekima Aliyoteremsha amebainisha kila kilicho na manufaaa kwa waja na kutengemaa kwa hali zao katika dini na dunia yao. Miiongoni mwa hayo ni I’tiqaad sahihi, matendo yaliyosalama, tabia nzuri na adabu iliyo juu. Akauacha (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) Ummah wake katika njia ilio wazi kabisa; usiku wake ni kama mchana wake na hakuna mwenye kuiacha isipokuwa mwangamivu.

Njia hii ikafuatwa na Ummah wake ambao umemuitikia Allaah na Mtume Wake. Wao, Maswahabah, Taabi’uun na wale waliowafuata kwa wema ndio viumbwe bora. Wakasimamisha Shari’ah yake, wakashikamana na Sunnah zake na wakaziuma kwa magego yao katika ‘Aqiydah, ‘ibaadah, tabia na adabu. Wao ndio walikuwa wale watu ambao daima ni wenye kushinda na wako wazi wazi juu haki. Hawawadhuru wale wenye kuwapinga na kwenda kinyume nao mpaka ije amri ya Allaah (Ta’ala) ilihali bado wako katika hali hiyo.

Sisi tunafuata nyayo zao na kwa msaada wa njia yao yenye kusapotiya na Kitabu na Sunnah tumeongoka - tunamshukuru Allaah kwa hilo. Tunasema

haya kwa kutaja neema ya Allaah (Ta’ala) aliyotutunukia na kubainisha yale ambayo ni wajibu kwa kila muumini kuwa juu yake.

Tunamuomba Allaah atuthibitishe sisi na ndugu zetu waislamu kwa kauli thabiti duniani na Aakhirah na atutunukie rahmah Zake - hakika Yeye ndiye mwingi wa Kutunuku.

Kutokana na umuhimu wa maudhui hii na kutofautiana kwa matamanio ya watu, nimependa kuandika kwa mukhtasari ‘Aqiydah yetu, ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa’ah. Imani hiyo ni kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, siku ya Mwisho na Qadar; kheri na shari yake. Ninamuomba Allaah (Ta’ala) ajaalie iwe *Khaalisw* kwa ajili ya Uso Wake, yenye kuafikiana na radhi Zake na yenye kuwanufaisha waja Wake.

‘Aqiydah yetu

‘Aqiydah yetu ni kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, siku ya Mwisho na Qadar; kheri na shari yake.

Tunaamini Uola wa Allaah (Ta’ala). Bi maana ya kwamba Yeye ndiye Mola, Muumbaji na Mfalme mwenye kuendesha mambo yote.

Tunaamini Uungu wa Allaah (Ta’ala). Bi maana Yeye ndiye Mungu wa haki na kila kinachoabudiwa badala Yake ni batili.

Tunaamini Majina na Sifa Zake, ina maana ya kwamba Yeye ana Majina mazuri na Sifa kamilifu zilizo kuu.

Tunaamini kuwa Yeye ni Mwenye kupwekeka katika mambo hayo. Bi maana hana mshirika katika Uola Wake, Uungu Wake wala katika Majina na Sifa Zake. Allah (Ta’ala) amesema:

رَبُّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا فَاعْبُدْهُ وَاصْطَبِرْ لِعِبَادَتِهِ ۝ هَلْ نَعْلَمُ لَهُ سَيِّئًا

"Mola wa mbingu na ardhi na vilivyo baina yake; basi mwabudu Yeye tu na dumisha subira katika ‘ibaadah Yake. Je, unamjua [mwengine] mwenye Jina kama Lake?"¹

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَقُّ الْقَيُّومُ ۝ لَا تَأْخُذُهُ سَيْنَةٌ وَلَا نَوْمٌ ۝ لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۝ مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ ۝ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفُهُمْ ۝ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ ۝ وَسَعَ كُرْسِيُّهُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ ۝ وَلَا يَمُودُهُ حِفْظُهُمْ ۝ وَهُوَ الْعَلِيُّ

الْعَظِيمُ

"Allaah, hakuna mungu wa haki ila Yeye, Aliyehai daima, Msimamizi wa kila kitu. Haumchukuwi usingizi wala kulala. Ni Vyake pekee vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi. Nani huyu ambaye anashufai [anayeombea] mbele Yake bila ya idhini Yake. Anajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Wala hawawezi kuzunguka chochote katika elimu Yake

¹ 19:65

isipokuwa kwa Alitakalo. Imeenea Kursiy Yake mbingu na ardhi. Wala hakumchoshi kuvihifadhi viwili hivyo. Naye ndiye Aliye juu, ndiye Mkuu."²

هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۖ عَالَمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ ۖ هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ ۖ هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْعَلِيُّ الْقَدُوسُ السَّلَامُ الْمُؤْمِنُ الْمُهَمِّسُ
الْعَزِيزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ ۚ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ۖ هُوَ اللَّهُ الْخَالِقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ ۖ لَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ۖ يُسَبِّحُ لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ
وَالْأَرْضِ ۖ وَمَوْعِدُ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

"Yeye ni Allaah, Ambaye hakuna mungu wa haki ila Yeye. Mjuzi wa yaliyofichikana na ya dhahiri, Yeye Ndiye Mwingi wa Rahmah, Mwenye kurehemu, Yeye Ndiye Allaah Ambaye hakuna mungu wa haki isipokuwa Yeye, Mfalme, Mtakatifu, Mwenye amani, Mwenye kusadikisha, Mwenye kutawala na kuendesha, Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima, Asiyeshindwa kufanya Atakalo, Mwenye kustahiki kiburi - Utakasifu ni wa Allaah kwa yale yote wanayomshirikisha nayo. Yeye Ndiye Allaah, Muumbaji, Mwanzishi viumbe bila kasoro, Mtengeneza sura, Ana Majina Mazuri kabisa, kinamtukuza Pekee kila kilichokuweko katika mbingu na ardhi - Naye Ndiye Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima, Mwenye hikmah wa yote daima."³

Tunaamini kuwa Allaah ndiye Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi:

لِلَّهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ يَعْلَمُ مَا يَشَاءُ ۖ يَهْبِطُ لِمَنْ يَشَاءُ إِنَّا وَهُنَّ بِهِ لِمَنْ يَشَاءُ الْذُكُورُ أَوْ يُرَوُّجُهُمْ دُكْرَانًا وَإِنَّا ۖ وَيَعْلَمُ مَنْ يَشَاءُ
عَقِيقًا ۖ إِنَّهُ عَلَيْهِ قَدِيرٌ

"Ni wa Allaah Pekee ufalme wa mbingu na ardhi. Anaumba Atakavyo. Humtunukia Amtakaye wana wa kike na Humtunukia Amtakaye wana wa kiime au Huwachanganya [wana wa] kiime na wa kike na Humjaalia Amtakaye kuwa ni tasa, hakika Yeye ni Mjuzi wa yote daima, Muweza wa yote daima."⁴

Tunaamini kuwa:

² 02:255

³ 59:22-23

⁴ 42:49-50

لَيْسَ كَوِيلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ^ك مَقَالِيدُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ يَسْطُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۖ إِنَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia yote daima, Mwenye kuona yote daima. Ni Zake Pekee funguo za mbingu na ardhi, Anamkunjulia riziki Amtakaye na Anamdhikisha [Amtakaye]. Hakika Yeye kwa kila kitu ni Mjuzi."⁵

وَمَا مِنْ ذَائِبٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رُرْقَهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَفَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا ۚ كُلُّهُ فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ

"Na hakuna kiumbe chochote katika ardhi isipokuwa riziki yake iko kwa Allaah; na Anajua makazi yake [tumboni mwa mama au duniani] na mahali pake pa kuhifadhiwa [baada ya kufa]. Yote yamo katika Kitabu kinachobainisha."⁶

وَعِنْهُ مَقَاتِعُ الْعَيْنِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ ۚ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ ۚ وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٌ فِي ظُلُمَاتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٌ وَلَا يَابِسٌ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ

"Na Kwake Pekee zipo funguo za mambo yaliyofichikana; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Anajua yale yote yaliyomo barani na baharini. Na halianguki jani lolote ila Hulijua. Na wala [haianguki] punje katika viza vya ardhi, na wala [hakianguki] kilichorutubika na wala [hakianguki] kikavu isipokuwa [kimeandikwa] katika Kitabu kinachobainisha."⁷

عِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَمُنْتَلِلُ الْعَيْنِ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْأَرْخَامِ ۖ وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ مَّا دَرَّبَتْهُ أَرْضٌ تَمُوتُ ۖ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ
حَسِيرٌ

"Ana elimu ya Qiyaamah, na Anateremsha mvua na Anajua yale yaliyomo katika matumbo, na nafsi yoyote haijui nini itachuma kesho, na nafsi yoyote haijui itafia katika ardhi gani, hakika Allaah ni Mjuzi wa yote daima, Mjuzi

⁵ 42:11-12

⁶ 11:06

⁷ 06:59

wa vilivyodhahiri na vilivyofichikana.”⁸

Tunaamini kuwa Allaah anazungumza kwa yale ayatakayo, pale anapotaka na namna anavyotaka:

وَكَلَمَ اللَّهُ مُوسَى تَكْلِيمًا

”Na bila shaka Allaah Alimsemesha Muwsaa maneno.”⁹

وَلَمَّا جَاءَ مُوسَى لِمِيقَاتِنَا وَكَلَمَ رُبْعَةً

”Na alipokuja Muwsaa katika miadi yetu, na Mola wake Akamsemesha.”¹⁰

وَنَادَيْنَاهُ مِنْ جَانِبِ الطُّورِ الْأَمْنِ وَقَرِبَتْنَاهُ حَجِيًّا

”Na Tukamwita kutoka upande wa kulia wa mlima na Tukamkurubisha kuzungumza naye kwa siri.”¹¹

Tunaamini kuwa:

لَوْ كَانَ الْبَحْرُ مَدَادًا لِكَلِمَاتِ رَبِّي لَنَفَدَ الْبَحْرُ قَبْلَ أَنْ تَنَفَدَ كَلِمَاتُ رَبِّي وَلَوْ چَنَّا بِعْثَلَهِ مَدَادًا

”Kama bahari ingelikuwa ni wino wa [kuandika] maneno ya Mola wangu, basi ingelimalizika bahari kabla ya kumalizika maneno ya Mola wangu, japokuwa Tungelileta [bahari ya] mfano wake kuwa wino.”¹²

وَلَوْ أَنَّمَا فِي الْأَرْضِ مِنْ شَجَرَةٍ أَقْلَامٌ وَالْبَحْرُ يَمْدُدُهُ مِنْ بَعْدِهِ سَبْعَةُ أَنْجُوْرٍ مَا نَفَدَتْ كَلِمَاتُ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

⁸ 31:34

⁹ 04:164

¹⁰ 07:143

¹¹ 19:52

¹² 18:109

"Na lau kama vile vyote vilivyomo ardhini kati ya miti [ingalikuwa] kalamu, na bahari [ikafanywa wino], ikaongezewa juu yake bahari saba [nyinginezo]; yasingelimalizika Maneno ya Allaah. Hakika Allaah ni Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima, Mwenye hikmah wa yote daima."¹³

Tunaamini kuwa Maneno Yake ni matimilifu ya kweli katika kueleza, adilifu katika hukumu na ni mazuri. Amesema (Ta’ala):

وَمَنْ كَلَمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا

"Na limetimia neno la Mola wako kwa kweli na uadilifu."¹⁴

وَمَنْ أَصْدَقَ مِنَ اللَّهِ حَدِيثًا

"Na nani mkweli zaidi katika maneno kuliko Allaah?"¹⁵

Tunaamini kuwa Qur-aan Tukufu ni Maneno ya Allaah (Ta’ala). Amezungumza kwayo kihakika na akamwacha Jibriyl ayachukie. Baada ya hapo Jibriyl akashuka nayo kwenye moyo wa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam).

فُلُونَ زَرَّاهُ رُوحُ الْقُدُسِ مِنْ رَبِّكَ بِالْحَقِّ لِيُبَيِّنَ الدِّينَ آمَنُوا وَهُدًى وُبُشِّرَى لِلْمُسْلِمِينَ وَلَقَدْ تَعْلَمُ أَنَّهُمْ يَقُولُونَ إِنَّمَا يُعَلِّمُهُ بَشَرٌ لِسَانُ الدُّجَى يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ أَنْجَحِيَّةٌ وَهَذَا لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُبِينٌ

"Sema: Ameiteremsha roho Mtakatifu [Jibriyl] kutoka kwa Mola wako kwa haki ili iwathibitishe wale walioamini na ni mwongozo na bishara kwa Waislamu. Na kwa yakini Tunajua kwamba wao [makafiri] wanasesma: "Hakika [kuna] mtu [ndiye] anamfundisha [huyu Muhammad]." Luga ya huyo wanayemnasibishia ni ya kigeni, na hii ni luga ya kiarabu bayana."¹⁶

¹³ 31:27

¹⁴ 06:115

¹⁵ 04:87

¹⁶ 16:102-103

وَإِنَّهُ لَتَنْزِيلُ رَبِّ الْعَالَمِينَ نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ عَلَى قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ يُلْسَانٌ عَرَبِيٌّ مُّبِينٌ

"Na hakika hiyo ni Uteremsho wa Mola wa walimwengu. Ameiteremsha haya roho Mwaminifu juu ya moyo wako [ee Muhammad] ili uwe mionganoni mwa waonyaji. Kwa lugha ya kiarabu bayana."¹⁷

Tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) Yuko juu ya viumbe Vyake kwa Dhati Yake na Sifa Zake. Amesema (Ta’ala):

وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ

"Naye ndiye Aliye juu, na ndiye Mkuu."¹⁸

وَهُوَ الْفَاعِلُ فَوْقَ عِبَادِهِ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْجَيِّرُ

"Naye ndiye Mwenye nguvu juu ya waja Wake; Nayé ni Mwenye hikmah wa yote daima, Mjuzi wa vilivyodhahiri na vilivyofichikana."¹⁹

خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سَيْةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَى عَلَى الْعَرْشِ يُدَبِّرُ الْأَمْرَ

"Ameumba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha akalingana juu ya ‘Arshi. Huyaendesha mambo."²⁰

Kulingana Kwake (Ta’ala) juu ya ‘Arshi ni kuwa Kwake juu yake kwa Dhati Yake. Ni Ujuu maalum wenye kulingana na Utukufu na Ukubwa Wake na hakuna anayejua namna yake isipokuwa Yeye peke yake.

Tunaamini kuwa Yeye (Ta’ala) Yuko pamoja na viumbe Vyake na wakati huo huo Yuko juu ya ‘Arshi Yake. Anazijua zali zao. Anayasikia maneno yao na

¹⁷ 26:192-195

¹⁸ 02:255

¹⁹ 06:18

²⁰ 10:03

anaona matendo yao. Anayaendesha mambo yao na anamruzuku fakiri. Anayarekebisha yenyе kuvunjika na anampa ufalme Amtakaye na anamwondolea ufalme Amtakaye. Anamtukuza amtakaye na kumwangusha amtakaye. Kheri iko Mikononi Mwake na Yeye juu ya kila jambo ni Muweza. Yule ambaye ana hadhi kama hii, anakuwa pamoja na waja Wake kihakika, hata kama atakuwa pia juu ya viumbe Vyake kihakika.

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia yote daima, Mwenye kuona yote daima.”²¹

Hatusemi kama wanavyosema Jahmiyyah na wakitaji (Huluuliyyah) wengine ya kwamba Allaah Yuko katika ardhi na viumbe Vyake. Tunaona kuwa mwenye kusema hivo ni kafiri au mpotevu, kwa sababu amemsifu Allaah kwa mapungufu yasiyolingana na Yeye.

Tunaamini yale Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) aliyomweleza kwayo ya kwamba Hushuka kila usiku kwenye mbingu ya dunia kunapobaki thuluthi ya usiku ya mwisho na anasema:

"Ni nani mwenye kuniomba du'aa Nimuitikie? Ni nani mwenye kuniomba Nimpe? Ni nani mwenye kuniomba msamaha Nimsamehe?"

Tunaamini kuwa Yeye (Ta’ala) atakuja siku ya Qiyaamah kuhukumu kati ya waja. Amesema (Ta’ala):

كَلَّا إِذَا دُكَّتِ الْأَرْضُ دَكَّا وَجَاءَ رِئَنُكَ وَالْمَلَكُ صَفَّا وَجْهِيَّةً يَوْمَئِذٍ بِهِنَّمَ ۝ يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ الْإِنْسَانُ وَأَنَّ لَهُ الدِّكْرِي

“Sivyo hivyo! [Kumbukeni pale] ardhi itakapovunjwavunjwa. Na Atakapokuja Mola wako na Malaika safusafu. Na utaletwa siku hiyo [Moto wa] Jahannam; siku hiyo mwanaadamu atakumbuka, lakini wapi atapata

²¹ 42:11

ukumbusho?”²²

Tunaamini kuwa Anafanya alitakalo:

فَعَالٌ لِمَا يُرِيدُ

“Afanyaye Alitakalo.”²³

Tunaamini kuwa Yeye (Ta’ala) ana Utashi aina mbili:

Wa kilimwengu (Kawniyyah): Kwa Utashi huo kunapitika yale anayoyataka. Pamoja na hivyo hailazimishi kwamba anayapenda. Katika hayo ni pamoja na Kauli Yake:

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا افْتَنَّهُ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ

“Na lau Angelitaka Allaah wasingelipigana lakini Allaah Anafanya Ayatakayo.”²⁴

إِنْ كَانَ اللَّهُ يُرِيدُ أَنْ يُعَذِّبَكُمْ هُوَ رَبُّكُمْ

“Ikiwa Allaah Anataka kukuacheni kupotea. Yeye ndio Mola wenu.”²⁵

Ya Kishari’ah (Shar’iyyah): Utashi huo haulazimishi yapitike yale anayoyataka. Pamoja na hivyo yanalazimisha kwamba yale yenye kupidika anayapenda. Amesema (Ta’ala):

وَاللَّهُ يُرِيدُ أَنْ يَتُوبَ عَلَيْكُمْ

²² 89:21-23

²³ 85:16

²⁴ 02:253

²⁵ 11:34

"Na Allaah Anataka kupokea tawbah kwenu."²⁶

Tunaamini kuwa Matakwa Yake ya kilimwengu na ya Kishari’ah ni yenyekutokamana na Hekima Yake. Kila Anachokipanga kilimwengu au Kishari’ah waja wakaabudu kwacho, kinatokamana na Hekima, sawa tuwe tunajua Hekima hiyo au hatujui:

أَلَيْسَ اللَّهُ بِأَحْكَمِ الْحَاكِيمَيْنَ

"Je, kwani Allaah si Mbora wa wanaohukumu?"²⁷

وَمَنْ أَخْسَنُ مِنَ اللَّهِ خَكْرًا لِّقَوْمٍ يُؤْتَفَوْنَ

"Na nani mbora zaidi kuliko Allaah katika kuhukumu; [Yanafahamika haya] kwa watu wenyewe yakini."²⁸

Tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) anawapenda mawalii Wake na wao wanampenda:

فُلُونَ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يَعْبِدُنِي اللَّهُ وَيَغْفِرُ لَكُمْ ذُنُوبُكُمْ وَاللَّهُ عَفُورٌ رَّحِيمٌ

"Sema: "Mkiwa mnampenda Allaah, basi nifuateni, Atakupendeni Allaah na Atakusameheni dhambi zenu. Na Allaah ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu."²⁹

فَسَوْفَ يَأْتِيَ اللَّهُ يَقْرُئُ يَعْبُدُهُمْ وَيُحِبُّهُنَّ

"Allaah Ataleta watu Atakaowapenda nao watampenda."³⁰

²⁶ 04:27

²⁷ 95:08

²⁸ 05:50

²⁹ 03:31

³⁰ 05:54

وَاللَّهُ يُحِبُّ الصَّابِرِينَ

"Na Allaah Anapenda wanaosubiri."³¹

وَأَفْسِطُوا ۝ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُفْسِطِينَ

"Na fanyeni haki. Hakika Allaah Anapenda wafanyao haki."³²

وَأَخْسِنُوا ۝ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ

"Na fanyeni wema Hakika Allaah Anapenda wafanyao wema."³³

Tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) anaridhia yale matendo na maneno Aliyoyaweka katika Shari’ah na kuchukia yale Aliyoyakataza:

إِن تَكُفُّرُوا فَإِنَّ اللَّهَ عَنِّي عَنْكُمْ ۝ وَلَا يَرْضَى لِعِبَادِهِ الْكُفُرُ ۝ وَإِن تَشْكُرُوا يَرْضَهُ لَكُمْ

"Mkikufuru, basi [eleweni kuwa] hakika Allaah ni Mkwasi kwenu na wala Haridhii kufuru kwa waja Wake. Na mkishukuru Huridhika nanyi."³⁴

وَلَكِنْ كَرِهُ اللَّهُ ابِيَّا ثُمَّ قَبَّطُهُمْ وَقَبِيلٌ افْعَدُوا مَعَ الْقَاعِدِينَ

"Lakini Allaah Amechukia kutoka kwao, basi Akawazuia na ikasemwa:
"Kaeni [mbakie majumbani] pamoja na wanaokaa."³⁵

Tunaamini kuwa Allaah Yuko radhi na wale wenye kuamini na kutenda matendo mema:

³¹ 03:146

³² 49:09

³³ 02:195

³⁴ 39:07

³⁵ 09:46

رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ ۚ ذَلِكَ لِمَنْ حَشِيَ رَبُّهُ

“Allaah Ataridhika nao, nao wataridhika Naye; hayo ni kwa yule anayemkhofu Mola wake.”³⁶

Tunaamini kuwa Allaah anawaghadhibikia makafiri na wengine wenye kustahiki kufanyiwa hivo:

الظَّاهِيْنَ بِاللَّهِ ظَاهِيْنَ السَّوْءَ ۚ عَلَيْهِمْ دَائِرَةُ السَّوْءِ ۖ وَعَصِيَّبَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ

“Wanaomdhania Allaah dhana ovu utawafikia mgeuko uovu; na Allaah Awaghadhibikie.”³⁷

مَنْ كَفَرَ بِاللَّهِ مِنْ بَعْدِ إِيمَانِهِ إِلَّا مَنْ أَكْرَهَ وَقَلْبُهُ مُطْمَئِنٌ بِالإِيمَانِ وَلَا كُنَّ مَنْ شَرَحَ بِالْكُفْرِ صَدْرًا فَعَلَيْهِمْ غَضَبٌ مِّنَ اللَّهِ وَكُنُّ عَذَابٌ عَظِيمٌ

“Atakayemkufuru Allaah baada ya iymaan yake [atapata adhabu] isipokuwa yule aliyetenzwa nguvu na huku moyo wake umetua juu ya iymaan. Lakini aliyekifungulia ukafiri kifua chake, basi hao juu yao ni ghadhabu kutoka kwa Allaah na watapata adhabu kuu.”³⁸

Tunaamini kuwa Allaah Yuko na Uso. Ni Wenye kusifika kwa Utukufu na Ukarimu:

وَبِيَقْنَى وَخْدُ رَبِّكَ دُوَ الْجَلَالِ وَالْكَرَامِ

“Na utabakia Uso wa Mola wako Mwenye utukufu na ukarimu.”³⁹

Tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) ana Mikono miwili mikunjufu na mikubwa:

³⁶ 98:08

³⁷ 48:06

³⁸ 16:106

³⁹ 11:37:39

بَلْ يَدَاهُ مَبْشُوتَانِ يُنْفِقُ كَيْفَ يَشَاءُ

"Bali Mikono Yake iwazi Hutoa Atakavyo."⁴⁰

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقًّا قَدْرِهِ وَالْأَرْضُ جَيْعًا قَبْضَتُهُ يَوْمُ الْقِيَامَةِ وَالسَّمَاءُ أَثْ مَطْوِيَّاتٌ بِمَمِينَهِ سُبْحَانَهُ وَتَعَالَى عَمَّا يُشْكُونَ

"Na hawakumthamini Allaah kama inavyostahiki kuthaminiwa; na ardhi yote Ataikamata [Mkononi Mwake] Siku ya Qiyaamah; na mbingu zitakunjwa Mkononi Mwake wa kulia. Utakasifu ni wa Allaah na Ametukuka kutokana na yale yote wanayomshirikisha."⁴¹

Tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) ana Macho mawili ya kihakika. Amesema (Ta’ala):

وَاصْنَعْ الْفُلْكَ بِأَعْيُنِنَا وَوَحْيَنَا

"Na unda jahazi mbele ya macho Yetu na ufunuzi wa Wahy Wetu."⁴²

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa’ah wamekubaliana juu ya kwamba Ana Macho mawili. Jambo lenye kutilia nguvu hilo ni kauli ya Mtume (Swalla Allaahu `alayhi wa sallam) kuhusu ad-Dajjal:

"Ana jicho moja na Mola Wenu hana Jicho moja."

Tunaamini kuwa:

لَا تُدِرِّكُ الْأَبْصَارُ وَهُوَ يُدِرِّكُ الْأَبْصَارَ وَهُوَ الْلَّطِيفُ الْحَسِيرُ

"Macho hayamzunguki bali Yeye Anayazunguka macho [yote]; Naye ni Mwenye kuyaendesha mambo kwa utuvu, Mjuzi wa vilivyodhahiri na

⁴⁰ 05:64

⁴¹ 39:67

⁴² 05:50

vilivyofichikana.”⁴³

Tunaamini kuwa waumini watamuona Mola Wao siku ya Qiyaamah:

وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ إِلَى رَّبِّهَا نَاطِرَةٌ

“[Kuna] nyuso siku hiyo zitanawiri. Zikimtazama Mola wake.”⁴⁴

Tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) hana wa kufanana Naye, kutokana na ukamilifu wa Sifa Zake:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia yote daima, Mwenye kuona yote daima.”⁴⁵

لَا تَأْخُذْهُ سِنَةٌ وَلَا نَوْمٌ

“Haumchukuwi usingizi wala kulala.”⁴⁶

Tunaamini kuwa hamdhulumu yoyote, kutokanana ukamilifu wa uadilifu Wake:

Vilevile tunaamini kuwa si Mwenye kughafili na matendo ya yejote katika waja Wake, kutokana na ukamilifu wa uchungaji na ujuzi Wake.

Tunaamini kuwa hakuna chenye Kumshinda mbinguni na ardhini, kutokana na ukamilifu wa ujuzi na uwezo Wake:

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ

⁴³ 06:103

⁴⁴ 75:22-23

⁴⁵ 42:11

⁴⁶ 02:255

"Hakika Amri Yake Akitaka kitu chochote, hukiambia: "Kuwa!" nacho huwa."⁴⁷

Hafikiwi na kitu kuchoka wala ushindwi, kutokana na ukamilifu wa nguvu Zake:

وَلَقَدْ خَلَقْنَا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ وَمَا مَسَّنَا مِنْ لُغُوبٍ

"Na kwa yakini Tumeumba mbingu na ardhi na vilivyo baina yake katika siku sita, na wala Haukutugusa uchovu wowote."⁴⁸

Bi maana hakuvisi kuchoka wala kutaabika.

Tunaamini kuthibiti Majina na Sifa zote ambazo Allaah amejithibitishia Mwenyewe, au Majina na Sifa alizomthibitishia Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Lakini hata hivyo tunajitenga mbali na mambo mawili ya khatari:

1. Kulinganisha kwa kuamini au kwa maneno Sifa za Allaah na sifa za viumbe.
2. Kuziwekea namna kwa kuamini au kwa maneno ya kwamba Sifa za Allaah (Ta’ala) ziko namna fulani.

Tunaamini Allaah kutokuwa na kila kitu ambacho amejikanushia kuwa nacho, au kitu ambacho Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amemkanushia kuwa nacho. ‘Aqiydah hiyo ndani yake mna kuthibitishia kilicho kinyume chake. Vilevile tunanyamazia yale aliyyoyanyamazia Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam).

Tunaona kuwa kushikamana na mfumo huu ni jambo la lazima. Yale ambayo Allaah amejithibitishia au kujikanushia Mwenyewe, ni maelezo ambayo Allaah amejithibitishia Mwenyewe. Yeye (Subhaanah) ni Mjuzi zaidi wa Nafsi Yake na

⁴⁷ 36:82

⁴⁸ 50:38

ni Mkweli zaidi wa usemi na ni Mwenye usemi mzuri kabisa, wakati waja Wake hawawezi kumzunguka kwa ujuzi. Vilevile yale aliyomthibitishia Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) au akamkanushia, ni maelezo aliyomweleza kwayo. Hakika yeye ni kiumbe mjuzi zaidi kuhusu Mola Wake, mtoaji nasaha, mwaminifu na mfaswaha zaidi.

Katika Maneno ya Allaah (Ta’ala) na Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) mna ujuzi kamilifu, ukweli na ubainifu zaidi. Hivyo hakuna udhuru kwa kuyarudisha au kuyatilia shaka kuyakubali.

Kumuamini Allaah

Yote tuliyoyataja kuhusiana na Sifa za Allaah (Ta’ala), kwa ufanuzi au kwa jumla, kuthibitisha au kukanusha, ni wenyewe kutegemea Kitabu cha Mola Wetu na Sunnah za Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) kwa mujibu wa ufahamu wa wahenga wa Ummah huu, maimamu wa Uongofu na wafuasi wao.

Kuhusiana na suala hili, tunaona kuwa ni wajibu kuyapitisha/kuyafasiri maandiko ya Qur-aan na Sunnah kwa udhahiri wake na kuyaamini uhakika wake kwa njia yenye kulingana na Allaah (‘Azza wa Jall).

Tunajitenga mbali na msimamo wa wale watu wenyewe msimamo wa kuyapindisha. Wameyefasiri kwa njia nyingine mbali na ile aliyokusudia Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam).

Vilevile tunajitenga mbali na wale watu waliyoyakanusha kwa ile maana aliyokusudia Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam).

Kadhalika tunajitenga mbali na wale watu waliyoyafasiri kwa njia yenye kuvuka mipaka na wakawa ima wameyafananisha au kuyawekea namna.

Tunajua kwa yakini ya kwamba yale yote yaliyokuja katika Kitabu cha Allaah (Ta’ala) au Sunnah za Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) ni haki na hayagongani:

أَفَلَا يَتَدَبَّرُونَ الْقُرْآنَ ۚ وَلَوْ كَانَ مِنْ عِنْدِ غَيْرِ اللَّهِ لَوْجَدُوا فِيهِ اخْتِلَافًا كَثِيرًا

"Je hawaizingatii Qur-aan? Na lau ingelikuwa imetoka kwa mwingine asiyekuwa Allaah, bila shaka wangelikuta ndani yake tofauti nyingi."⁴⁹

Kupatikana mgongano humo, kunalazimisha baadhi ya maandiko kukadhibisha mengine - na hili ni jambo lisilowezekana katika maelezo ya Allaah (Ta’ala) na maelezo ya Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Mwenye kudai kuwa

⁴⁹ 04:82

katika Kitabu cha Allaah au Sunnah za Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) kuna kitu kujigonga, hilo linatokamana na makusudio yake mabaya na ni kwa sababu ana moyo uliyopinda. Kwa ajili hiyo anatakiwa kutubu kwa Allaah (Ta’ala) au kuigeuzia dhambi yake mgongo.

Hata hivyo yule mwenye kufikiri kuwa katika Kitabu cha Allaah (Ta’ala), Sunnah za Mtume Wake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) au kati yavyo viwili kuna mgongano, hilo linatokamana ima na udogo wa elimu yake, ufahamu wake mpungufu au ufupi wa kuzingatia kwake. Kwa hivyo mtu kama huyo anatakiwa kutafuta elimu na azingatie kwa kina mpaka haki iweze kumbainikia. Ikiwa mambo hayakumbainikia, basi ampasie jambo hilo mwalimu wake, akomeke na fikira zake na aseme yale wanayosema waliobobea katika elimu:

آمَّا بِهِ كُلُّ مِنْ عِنْدِ رَبِّنَا

“Tumeziamini, zote ni kutoka kwa Mola wetu.”⁵⁰

Pamoja na hivyo anatakiwa kujua kuwa katika Qur-aan na Sunnah hakuna kabisa hakujigonga na hii haigongi nyingine wala hakuna kutofautiana kati yavyo.

⁵⁰ 03:07

Kuwaamini Malaika

Tunawaamini Malaika wa Allaah (Ta’ala) na kwamba:

عِبَادُ مُكْرِمُونَ لَا يَسْتَغْوِنُهُ بِالْقُوَّلِ وَهُمْ بِأَمْرِهِ يَعْمَلُونَ

“Ni waja waliokirimiwa. Hawamtangulii [Allaah] kwa kauli, nao kwa amri Yake wanafanya.”⁵¹

Allaah (Ta’ala) amewaumba na wanamuabudu na kumtii kwa kumnyenyeka:

لَا يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِهِ وَلَا يَسْتَحْسِرُونَ يُسْبِحُونَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لَا يَفْتَرُونَ

“Hawatakabari na ‘ibaadah Yake na wala hawachoki. Wanamtukuza usiku na mchana, wala hawazembei.”⁵²

Allaah ametuficha nao na kwa ajili hiyo hatuwaoni. Hata hivyo kuna uwezekano baadhi ya waja wakawaona. Kwa mfano Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alimuona Jibriyl (‘alayhis-Salaam) katika umbile lake la asli. Alikuwa na mbawa mia sita zilizokuwa zimefunika upeo wa juu wote. Kadhalika alijifananisha katika umbile sawa na mtu wakati alipomshukia Maryam. Jibriyl akazungumza naye na Maryam na yeye akazungumza naye. Vilevile siku moja alikuja kwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) na Maswahabah zake katika umbile la mtu. Walikuwa hawamjui mtu huyo; hakuwa na alama yenye kuonesha kuwa ni msafiri na alikuwa na nguo nyeupe pee na nywele zake zilikuwa nyeusi sana. Akakaa kandoni na Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam), akaweka magoti yake karibu na magoti ya Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) na akaweka vitanga vyake juu ya magoti yake. Akazungumza na Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) na Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akazungumza naye. Baada ya hapo Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) akazungumza naye.

⁵¹ 21:26-27

⁵² 21:19-20

wa sallam) akawaeleza Maswahabah zake ya kwamba mtu yule alikuwa ni Jibriyl.

Tunaamini kuwa Malaika wamelazimishwa kazi mbali mbali.

Jibriyl amewakilishwa kuteremsha *Wahyi* kuutoa kwa Allaah na kumteremshia Nabii na Mtume amtakaye.

Mikaaiyl amewakilifishwa mvua na mazao.

Israafiyel amewakilishwa kupuliza baragumu itapofika wakati wa Kuzimia na Kufufuliwa.

Malaika wa mauti amewakilishwa kuzichukua roho za watu inapofika wakati wa mauti.

Malaika wa mlima amewakilishwa na mlima.

Malaika Maalik ambaye ni mlinzi wa Moto.

Kuna Malaika waliowakilishwa na vipomoko kwenye vifuko vya uzazi. Kuna Malaika wengine wamewakilishwa kumhifadhi mwanaadamu, wengine wamewakilishwa kuandika matendo yao, kwa sababu kila mtu ana Malaika wawili:

إِذْ يَنَلُّ الْمُتَّلَقِيَانَ عَنِ الْبَيْنِ وَعَنِ الشَّمَالِ قَعِيدٌ مَا يُلْفَظُ مِنْ قَوْلٍ إِلَّا لَدَنِهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ

“Pale wanapopokea wapokeaji wawili wanaokaa kuliani na kushotoni. Hatamki kauli yejote ile isipokuwa yuko karibu naye mwangalizi amejitayarisha [kurekodi].”⁵³

Kadhalika kuna Malaika waliowakilishwa kumuhoji maiti. Pale ambapo maiti ameshawekwa kwenye mwana-ndani, anajija na Malaika wawili na wanamuuliza kuhusu Mola Wake, dini Yake na Mtume Wake.

⁵³ 50:17-18

يُبَشِّرُ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا بِالْقُوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ۖ وَيُعَذِّلُ اللَّهُ الظَّالِمِينَ ۖ وَيَفْعَلُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ

"Allaah Huwathibitisha wale walioamini kwa kauli thabiti katika uhai wa dunia na Aakhirah. Na Allaah Huwaacha kupotoka madhalimu. Na Allaah Anafanya Atakavyo."⁵⁴

Kuko Malaika waliowakilishwa na watu wa Peponi:

وَالْمَلَائِكَةُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِمْ مِنْ كُلِّ بَابٍ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ ۖ فَنَعَمْ عُفْيَ الدَّارِ

"Na Malaika wanawaingilia katika kila milango [na kusema] "Salaamun 'Alaykum" [Amani iwe juu yenu] kwa yale mliyosubiri. Basi uzuri ulioje hatima [nzuri] ya nyumba [ya Aakhirah]."⁵⁵

Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) ameeleza kuwa Nyumba inayozuriwa mbinguni huingia (na katika upokezi mwagine "huswali ndani yake") kwa kila siku moja Malaika elfu sabini kisha baada ya hapo hakuna katika wao anayerudi tena.

⁵⁴ 14:27

⁵⁵ 13:23-24

Kuamini Vitabu

Tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) ameteremsha Vitabu ambavyo ni hoja dhidi ya viumbe na ni hoja kwa waumini. Kwavyo, wanawafunza hekima na kuwatakasasa.

Tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) amemteremshia kila Mtume Kitabu. Amesema (Ta’ala):

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْبَيِّنَاتِ لِيَتُّمَّمَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ

“Kwa yakini Tuliwapeleka Mitume Wetu kwa hoja bayana na Tukateremsha pamoja nao Kitabu na mizani ili watu wasimamie uadilifu.”⁵⁶

Miongoni mwa Vitabu hivyo tunajua vifuatavyo:

1. Tawraat ambayo Allaah (Ta’ala) amemteremshia Muusa (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Tawraat ndio Kitabu kikubwa kwa wana wa Israaiyl.

فِيهَا هُدًى وَنُورٌ يَحْكُمُ بِهَا النَّبِيُّونَ الَّذِينَ أَسْلَمُوا لِلَّهِ دِينُهُمْ وَالرَّبَّانِيُّونَ وَالْأَخْبَارُ إِمَّا اسْتُخْفِظُوا مِنْ كِتَابِ اللَّهِ وَكَانُوا عَلَيْهِ شُهَدَاءٍ

"Humo mna mwongozo na nuru ambayo kwayo, Manabii waliojisalimisha [kwa Allaah] waliwahukumu Mayahudi na watawa na wanazuoni wa kiyahudi pia [walihukumu kwa hiyo Tawraat] kwa sababu waliyokabidhiwa kuhifadhi Kitabu cha Allaah; na wakawa mashahidi juu yake."⁵⁷

2. Injiyl ambayo Allaah (Ta’ala) amemteremshia Iysaa (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Inaisadikisha Tawraat na kuikamilisha.

وَآتَيْنَاهُ الْإِنجِيلَ فِيهِ هُدًى وَنُورٌ وَمُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدِيهِ مِنَ التَّوْرَاةِ وَهُدًى وَمُؤْعِظَةٌ لِلْمُتَّقِينَ

⁵⁶ 57:25

⁵⁷ 05:44

"Na Tukampa Injiyl iliyomo ndani yake mwongozo na nuru; na isadikishayo yale yaliyokuwa kabla yake katika Tawraat, na ni mwongozo na mawaidha kwa wenyewe taqwa.⁵⁸

وَلِأَحِلَّ لَكُمْ بَعْضَ الَّذِي حُرِّمَ عَلَيْكُمْ

"Ili nikuhalalishi ni baadhi ya yale yaliyoharamishwa kwenu."⁵⁹

3. Zabuur ambayo Allaah (Ta’ala) amempa Daawuud (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam).
4. Suhuf ya Ibraahiyim na Muusa (‘alayhimaas-Salaam).
5. Qur-aan Kubwa ambayo Allaah (Ta’ala) amemteremshia Mtume wa mwisho Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam).

هُدًى لِلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَىٰ وَالْفُرْقَانِ

"Ili iwe mwongozo kwa watu na hoja bayana za mwongozo na pambanuo."⁶⁰

مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتَابِ وَمُهَمِّمًا عَلَيْهِ

"Kinachosadikisha yale [yaliyokuja katika] Vitabu vilivyokuwa kabla yake na kuvihukumia."⁶¹

Allaah amevifuta Vitabu vyote vilivytangulia kwa Qur-aan na Akachukua jukumu la kuihifadhi na mchezo wa wachezaji na upindaji wa wapindaji.

⁵⁸ 05:46-47

⁵⁹ 03:50

⁶⁰ 02:185

⁶¹ 05:48

إِنَّا نَحْنُ نَرْتَلُ الدِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ

"Hakika Sisi ndio Tumeteremsha Ukumbusho [huu] na Sisi bila shaka ndio Tutakaoihifadhi."⁶²

Itaendelea kubaki kuwa ni hoja juu ya viumbe vyote mpaka siku ya Qiyaamah.

Ama kuhusu Vitabu vilivyotangulia, ni vya muda fulani mpaka kunaposhuka Uteremsho wenyewe kuvifuta na kubainisha yaliyopotoshwa humo na kubadilishwa. Kwa ajili hiyo ndio maana havikuhifadhiwa na hivyo vikapotoshwa, vikazidishwa na kupunguzwa:

مِنَ الَّذِينَ هَادُوا يُخْرِجُونَ الْكِلَمَ عَنْ مَوَاضِعِهِ

"Katika Mayahudi wako wanaobadilisha maneno kuyatoa mahali pake"⁶³

فَوَيْلٌ لِّلَّذِينَ يُخْتَبِئُونَ الْكِتَابَ بِأَيْدِيهِمْ ثُمَّ يَقُولُونَ هَذَا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ لَيَسْتُرُوا بِهِ مَمَّا كَبَثَ أَيْدِيهِمْ وَوَيْلٌ لَّهُمْ بِمَا يَكْسِبُونَ

"Basi ole kwa wale wenyewe kuandika kitabu kwa mikono yao; kisha wakasema: "Haya ni kutoka kwa Allaah" ili wayabadilishe kwa thamani ndogo. Basi ole wao kwa yale yaliyoandikwa na mikono yao, na ole wao kwa yale wanayoyachuma."⁶⁴

فَلَمَّا مَنْ أَنْزَلَ الْكِتَابَ الَّذِي جَاءَ بِهِ مُوسَى نُورًا وَهُدًى لِلنَّاسِ بَعْجَلُوهُ قَرَاطِيسٍ ثُبُدوْنَهَا وَخُلُقُونَ كَثِيرًا

"Nani aliyeteremsha Kitabu ambacho amekuja nacho Muwsaa, [chenye] nuru na mwongozo kwa watu. Mnakifanya kurasa kurasa mkizifichua na mkificha mengi."⁶⁵

⁶² 15:09

⁶³ 04:46

⁶⁴ 02:79

⁶⁵ 06:91

وَإِنْ مِنْهُمْ لَفِرِيقًا يَلْكُونَ أَسْتَهْمَ بِالْكِتَابِ لِتَحْسِبُوهُ مِنَ الْكِتَابِ وَمَا هُوَ مِنَ الْكِتَابِ وَيَقُولُونَ هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَمَا هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبُ وَهُمْ يَعْلَمُونَ مَا كَانَ لِيَشِيرُ إِنْ يُؤْتِيَ اللَّهُ الْكِتَابَ وَالْحُكْمَ وَالنُّبُوَّةَ ثُمَّ يَقُولُ لِلنَّاسِ كُوْنُوا عِبَادًا لِي مِنْ دُونِ اللَّهِ

"Na hakika mionganoni mwao kuna kundi wanaopinda ndimi zao kwa [kusoma] Kitabu ili mdhanie kuwa hayo ni yanayotoka katika Kitabu na hali hayo si yenye kutoka katika Kitabu, na wanasema: "Hayo ni kutoka kwa Allaah"; na hali hayo si kutoka kwa Allaah na wanamsingizia uongo Allaah na wao wanajua. Haiwi kwa mtu [aliye Rasuli] kwamba Allaah Amempa Kitabu na hukumu na Unabii kisha awaambie watu: "Kuweni wenye kuniabudu mimi badala ya Allaah"⁶⁶

يَا أَهْلَ الْكِتَابِ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ كَثِيرًا مَا كُنْتُمْ تُخْفِونَ مِنَ الْكِتَابِ

"Enyi watu wa Kitabu! Hakika amekwishakujieni Mtume Wetu anayekubainishieni mengi katika yale mliyokuwa mkiyaficha katika Kitabu."⁶⁷

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ

"Kwa yakini wamekufuru wale waliosema: "Hakika Allaah Ndiye *al-Masiyh* mwana wa Maryam."⁶⁸

⁶⁶ 03:78-79

⁶⁷ 05:15

⁶⁸ 05:17

Kuamini Mitume

Tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) amewatumia viumbe Wake Mitume:

رُسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لَقَدْ يَكُونُ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةً بَعْدَ الرُّسُلِ ۝ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا

"Mitume ni wabashiriaji na waonyaji ili pasikuweko kutoka kwa watu hoja yoyote juu ya Allaah baada ya [kuletwa] Mitume. Na Allaah daima ni Mwenye enzi ya nguvu Asiyeshindika daima, Mwenye hikmah wa yote daima."⁶⁹

Tunaamini kuwa wa mwanzo wao ni Nuuh na wa mwisho wao ni Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam):

إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَيْ نُوحٍ وَالنَّبِيِّنَ مِنْ بَعْدِهِ

"Hakika Tumekufunulia Wahy kama Tulivyomfunulia Wahy Nuwh na Manabii baada yake."⁷⁰

مَّا كَانَ مُحَمَّدُ أَبَا أَخِيهِ مِنْ رِجَالِكُمْ وَلَكِنْ رَسُولَ اللَّهِ وَحَامِلُ النَّبِيِّنَ

"Hakuwa Muhammad baba wa mmoja yejote mionganoni mwa wanaume wenu, lakini ni Mtume wa Allaah na ni mwisho wa Manabii."⁷¹

Mbora wao wa kwanza ni Muhammad, kisha Ibraahiyim, kisha Muusa, kisha Nuuh na halafu Iysaa, mwana wa Maryam. Wamekhusishwa katika Kauli Yake (Ta’ala):

وَإِذْ أَخْدُنَا مِنَ النَّبِيِّنَ مِيقَاتَهُمْ وَمِنْكَ وَمِنْ نُوحٍ وَإِبْرَاهِيمَ وَمُوسَى وَعِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ ۝ وَأَخْدُنَا مِنْهُمْ مِيقَاتًا عَلَيْهِنَّ

"Na [kumbusha pale] Tulipochukua kutoka kwa Manabii fungamano yao na

⁶⁹ 04:165

⁷⁰ 04:163

⁷¹ 33:40

kutoka kwako, na kutoka kwa Nuwh, na Ibraahiyim, na Muwsaa, na ‘Iysaa mwana wa Maryam; na Tukachukua kutoka kwao fungamano gumu.”⁷²

Tunaamini kuwa Shari’ah ya Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) ina kheri zote inayopatikana katika Shari’ah za Mitume hawa wa kipekee. Amesema (Ta’ala):

شَرَعْ لَكُمْ مِنَ الدِّينِ مَا وَصَّى بِهِ نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَى وَعِيسَى ۖ أَنْ أَفِيمُوا الدِّينَ وَلَا تَنْقِرُّو فِيهِ

“Amekuamuruni katika Dini yale Aliyomuusia kwayo Nuwh, na ambayo Tumekuletea Wahy na Tuliyomuusia kwayo Ibraahiyim, na Muwsaa na ‘Iysaa kwamba: “Simamisheni Dini na wala msifarikiane ndani yake.”⁷³

Tunaamini kuwa Mitume wote ni wanaadamu walioumbwa. Hawana sifa hata moja ya Uungu. Amesema (Ta’ala) kuhusiana na Nuuh, ambaye ndiye wa kwanza wao:

وَلَا أَقُولُ لَكُمْ عِنْدِي حَرَائِنُ اللَّهِ وَلَا أَعْلَمُ الْعَيْبَ وَلَا أَقُولُ إِلَيْيَ مَلَكٍ

“Na wala sikuambieni kwamba mimi nina hazina za Allaah, na wala sijui ya ghayb na wala sikuambieni kwamba mimi ni Malaika.”⁷⁴

Allaah (Ta’ala) amemwamrisha Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam), ambaye ndiye wa mwisho wao, aseme:

لَا أَقُولُ لَكُمْ عِنْدِي حَرَائِنُ اللَّهِ وَلَا أَعْلَمُ الْعَيْبَ وَلَا أَقُولُ لَكُمْ إِلَيْيَ مَلَكٍ

“Sikuambieni kuwa mimi nina hazina ya Allaah; na wala kwamba najua

⁷² 33:07

⁷³ 42:13

⁷⁴ 11:31

mambo ya ghayb na wala sikuambieni kuwa mimi ni Malaika.⁷⁵

لَا أَمْلِكُ لِنَفْسِي نَفْعًا وَلَا ضَرًّا إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ

"Sema: "Siimilikii nafsi yangu manufaa yoyote wala dhara yoyote isipokuwa Apendavyo Allaah."⁷⁶

قُلْ إِنِّي لَا أَمْلِكُ لَكُمْ كُنْهًا ضَرًّا وَلَا رَشْدًا

"Sema: "Hakika mimi sikumilikieni dhara na wala uongofu."⁷⁷

Tunaamini kuwa ni waja miongoni mwa waja wa Allaah ambaa Allaah (Ta’ala) amewakirimu kwa ujumbe. Amewasifu kuwa ni waja wenye upeo wa juu na kadhalika Amewasifu. Amesema kuhusiana na wa mwanzo wao, Nuuh:

ذُرِّيَّةٌ مَنْ حَمَلْنَا مَعَ ثُوْجَةٍ إِنَّهُ كَانَ عَبْدًا شَكُورًا

"Kizazi [cha wale] Tuliowabeba pamoja na Nuwh [katika jahazi]! Hakika yeye alikuwa mja mwenye shukurani."⁷⁸

Amesema kuhusu wa mwisho wao, Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam):

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَى عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا

"Amebarikika Yule Ambaye Ameteremsha Pambanuzi kwa mja Wake ili awe muonyaji kwa walimwengu."⁷⁹

⁷⁵ 06:50

⁷⁶ 07:188

⁷⁷ 72:21

⁷⁸ 17:03

⁷⁹ 25:01

Kadhalika amesema kuhusu Mitume wengine:

وَادْكُرْ عَبْدَنَا إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ أُولَى الْأَئِدِي وَالْأَبْصَارِ

"Na [taja] waja Wetu; Ibraahiyim, na Is-haaq, na Ya’quwb, wenyengetu na utambuzi."⁸⁰

وَادْكُرْ عَبْدَنَا دَاؤُودَ ذَا الْأَئِدِي ﷺ إِنَّهُ أَوَّابٌ

"Na taja mja Wetu Daawuwd mwenye nguvu, hakika yeye ni mwenye kurudia rudia kutubu [kwa Allaah]."⁸¹

وَوَهَبْنَا لِدَاؤُودَ سُلَيْمَانَ َ نِعْمَ الْعَبْدُ ﷺ إِنَّهُ أَوَّابٌ

"Na Takamtunuku Daawuwd [mtoto] Sulaymaan; uzuri ulioje wa mja! Hakika yeye ni mwenye kurudia rudia kutubu [Kwetu]."⁸²

Vilevile amesema juu ya ‘Iysaa, mwana wa Maryam:

إِنْ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ وَجَعَلْنَا مَثَلًا لِّتَبَيَّنَ إِسْرَائِيلَ

"Yeye si chochote isipokuwa tu ni mja Tuliyemneemesha, na Tukamjaalia [kuwa ni] mfano kwa wana wa Israaiyl."⁸³

Tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) amekhitimisha ujumbe kwa ujumbe wa Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Amemtuma kwa watu wote. Amesema (Ta’ala):

⁸⁰ 38:45

⁸¹ 38:17

⁸² 38:30

⁸³ 43:59

فَلَنْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِلَيْ رَسُولِ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَبِيعًا الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُنْحِي وَيُمْبِثُ ۖ فَآمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ النَّبِيِّ الْأَكْرَمِيِّ الَّذِي يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَكَلِمَاتِهِ وَاتَّبِعُوهُ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ

"Sema: "Hakika mimi ni Mtume wa Allaah kwenu nyinyi nyote. [Allaah] Ambaye Pekee Anao ufalme wa mbingu na ardhi. Hakuna mungu wa haki ila Yeye - Anahuisha na Anafisha. Basi mwaminini Allaah na Mtume Wake, Nabii asiyejua kusoma na kuandika ambaye anamwamini Allaah na maneno Yake, na mfuateni ili mpate kuongoka."⁸⁴

Tunaamini kuwa Shari‘ah yake (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) ni dini ya Uislamu ambayo Allaah (Ta‘ala) amewaridhia nayo waja Wake. Allaah (Ta‘ala) hakubali kutoka kwa yejote dini isiyokuwa Uislamu. Amesema (Ta‘ala):

إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ

"**Hakika Dini mbele ya Allaah ni Uislamu.**"⁸⁵

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِيْنَكُمْ وَأَتَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيَتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِيْنًا

"**Leo Nimekukamilishieni dini yenu na Nimekutimizieni neema Yangu na Nimekuridhieni kwenu Uislamu uwe dini yenu.**"⁸⁶

وَمَنْ يَتَّبِعْ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِيْنًا فَلَنْ يُثْبَلْ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ

"**Na yejote anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitokubaliwa kwake; naye katika Aakhirah atakuwa mionganoni mwa waliokhasirika.**"⁸⁷

⁸⁴ 07:158

⁸⁵ 03:19

⁸⁶ 05:03

⁸⁷ 03:35

Tunaona kuwa mwenye kudai kuwa Allaah anakubali dini nyingine mbali na Uislamu, kwa mfano uyahudi au unaswara, ni kafiri. Mtu huyo anatakiwa kutubia au auwe hali ya kuwa ni mwenye kuritadi, kwa sababu ameikadhibisha Qur-aan.

Tunaona kuwa mwenye kukanusha ujumbe wa Muhammad (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) kwamba umetumilizwa kwa watu wote basi amewakanusha Mitume wote, hata yule Mtume ambaye atakuwa anadai kuwa anamuamini na kumfuata. Amesema (Ta’ala):

كَدَّبُتْ قَوْمٌ بِّوْحِ الْمَرْسَلِينَ

"Watu wa Nuwh walikadhibisha Mitume."⁸⁸

Amesema kuwa wamekadhibisha Mitume wote, pamoja na kuwa hakukutanguliwa kuwepo na Mtume kabla ya Nuuh:

إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَيُرِيدُونَ أَنْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَيَقُولُونَ نُؤْمِنُ بِعَضٍ وَنَكْفُرُ بِعَضٍ وَيُرِيدُونَ أَنْ يَتَّخِذُوا بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا أُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ حَمَّا وَأَعْنَدُنَا لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُهِينًا

"Hakika wale waliomkanusha Allaah na Mtume Wake; na wanataka kufarikisha baina ya Allaah na Mtume Wake na wanasem: "Tunaamini baadhi [ya Mitume] na tunawakanusha baadhi" na wanataka kuchukua njia iliyo baina [kati kati] ya hayo - hakika hao ndio makafiri wa kweli. Na Tumewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha."⁸⁹

Tunaamini kuwa hakuna Nabii yoyote baada ya Muhammad Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Kwa hiyo yule mwenye kudai kuwa ni Nabii baada yake au akamsadikisha mwenye kuja na madai hayo, ni kafiri, kwa sababu anamkadhibisha Allaah, Mtume Wake na maafikiano ya waislamu.

⁸⁸ 26:105

⁸⁹ 04:150-151

Tunaamini kuwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) ana makhaliyfah waongofu. Wamechukua uongozi baada yake na kuuongoza Ummah wake kwa ujuzi, propaganda na uongozi na mamlaka juu ya waislamu. Mbora wao ni Abu Bakr as-Swiddiyq. Yeye ndiye mwenye haki zaidi ya ukhaliyfah. Kisha anafuata ‘Umar bin al-Khattaab, ‘Uthmaan bin ‘Affaan na kisha ‘Aliy bin Abiy Twaalib (Radhiya Allaahu ‘anhuma).

Namna hii ndivyo zilivyo fadhila zao, na pia ndivyo ustahiki wao wa kuongoza ulivyo. Allaah (Ta’ala) - na Yeye ana Hekima kubwa - katu asingelimwacha mtu kuongoza karne bora, lau kama kungelikuwa mwagine ambaye ni bora zaidi na mwenye kustahiki zaidi ukhaliyfah.

Tunaamini pia kuwa mmoja katika watu hawa anaweza kuwa na sifa ya kipekee yenye kumfanya akawa ni bora kuliko yule ambaye ni mbora zaidi kuliko yeye kwa jumla. Lakini hata hivyo haina maana ya kwamba anastahiki fadhila za moja kwa moja juu ya yule mwenye kumshinda, kwa sababu kuna mambo mengi mbali mbali yanayopelekea katika fadhila.

Tunaamini kuwa Ummah huu ndio Ummah bora na mtukufu zaidi kwa Allaah (‘Azza wa Jall). Amesema (Ta’ala):

كُنْتُمْ خَيْرُ أُمَّةٍ أَخْرَجْتُ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَيُونَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ

"Mmekuwa Ummah bora kabisa uliotolewa kwa watu: mnaamrisha mema na mnakataza munkari na mnawamini Allaah."⁹⁰

Tunaamini kuwa wabora wa Ummah huu ni Maswahabah, kisha Taabi’uun na halafu waliokuja baada yao.

Tunaamini kuwa kutakuwepo siku zote kikundi katika Ummah huu kilicho juu ya haki wazi wazi. Hakidhuriki na wale wenye kuwapinga na wenye kwenda kinyume nao mpaka ije amri ya Allaah (‘Azza wa Jall).

⁹⁰ 03:110

Tunaitakidi kuwa matatizo yaliyotokea kati ya Maswahabah ilikuwa ni kwa sababu ya mitazamo waliokuwa wakionelea kuwa ni ya sawa. Aliyepatia anapata thawabu mara mbili na mwenye kukosea anapata thawabu mara moja na kosa ni lenye kusamehewa.

Tunaona kuwa ni wajibu kunyamazia makosa yao. Hivyo hatuwataji isipokuwa tu kwa njia na sifa nzuri wanazostahiki. Tunaisafisha mioyo yetu kutokana na vifundo na chuki kwao. Amesema (Ta’ala):

لَا يَسْتَوِي مِنْكُمْ مَنْ أَنْفَقَ مِنْ قَبْلِ الْفَتحِ وَقَاتَلَ ۚ وَلِكُلِّ أَعْظَمٍ دَرْجَةٌ مِنَ الَّذِينَ أَنْفَقُوا مِنْ بَعْدِ وَقَاتَلُوا ۚ وَكُلُّاً وَعْدَ اللَّهِ الْحَسِنَىٰ

“Hawi sawa miongoni mwenu aliyetao kabla ya Ushindi [wa Makkah] na akapigana. Hao watapata daraja kubwa kabisa kuliko wale waliota baada [ya ushindi] na wakapigana - na wote Allaah Amewaaahidi Pepo.”⁹¹

Kadhalika amesema (Ta’ala) juu yetu:

وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَغْفِرْ لَنَا وَلَا حُوَانِّا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِإِيمَانٍ وَلَا يَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلَّا لِلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

“Na wale waliokuja baada yao [ni wenye] kusema: “Mola wetu! Tusamehe na ndugu zetu ambao wametutangulia kwa iymaan na wala Usijaalie katika nyoyo zetu mafundo kwa wale walioamini. Mola wetu! Hakika Wewe ni Mwenye huruma mno, Mwenye kurehemu.”⁹²

⁹¹ 57:10

⁹² 59:10

Kuamini siku ya Qiyaamah

Tunaamini siku ya Mwishes ambayo ni siku ya Qiyaamah. Hakuna siku baada yake. Siku hiyo watu watafufuliwa ilihali wako hai kwa ajili ya maisha ya milele. Makazi yao ya mwishes itakuwa ima ni Peponi au Motoni.

Tunaamini Kufufuliwa ambapo Allaah atawahuisha maiti. Hili litapitika pale ambapo Israafiyel atapopuliza baragumi kwa mara ya pili:

وَنُفَخَ فِي الصُّورِ فَصَعَقَ مَنِ فِي السَّمَاوَاتِ وَمَنِ فِي الْأَرْضِ إِلَّا مَنْ شَاءَ اللَّهُ أَلْمَمْ نُفَخَ فِيهِ أُخْرَى فَإِذَا هُنْ قِيَامٌ يَنْظُرُونَ

"Na itapulizwa baragumu; watazimia wale walioko mbinguni na ardhini isipokua Amtakaye Allaah. Kisha litapulizwa humo mara nyingine, tahamaki hao wanasmama wakitazama."⁹³

Watu watainuka kutoka kwenye makaburi yao kwa ajili ya Mola wa walimwengu. Watakuwa miguu peku, uchi na bila ya kutahiriwa:

كَمَا بَدَأْنَا أَوَّلَ حَلْقٍ تُعِيدُهُ ۝ وَعَدَّا عَلَيْنَا ۝ إِنَّا كُنَّا فَاعِلِينَ

"Kama Tulivyoanza [uumbaji] umbo la awali Tatalirudisha. Hii ni ahadi juu Yetu. Hakika Sisi Tumekuwa ni Wenye kufanya [Tuyasemayo]."⁹⁴

Tunaamini Madaftari ya matendo. Yatagawiwa kwa mkono wa kulia au nyuma ya mgongo [upande wa] kushoto:

فَأَمَّا مَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِيمِينِهِ فَسَوْفَ يُحَاسَبُ حِسَابًا يَسِيرًا وَيَنْقَلِبُ إِلَى أَهْلِهِ مَسْرُورًا وَأَمَّا مَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ وَرَاءَ ظَهِيرَهُ فَسَوْفَ يَدْعُو شُبُورًا وَيَصْلَى سَعِيرًا

"Basi ama yule atakayepewa kitabu chake kuliani mwake, basi atahesabiwa hesabu nyepesi na atageuka kwa ahli zake akiwa mwenye furaha. Na ama yule atakayepewa kitabu chake nyuma ya mgongo wake, basi ataomba maangamizi

⁹³ 39:68

⁹⁴ 21:104

na ataingia aungue [Moto wa] *Sa’iyraa.*⁹⁵

وَكُلَّ إِنْسَانٍ أَلْرَمَنَاهُ طَائِرٌ فِي عَنْقِهِ ۝ وَخُرْجَ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ كِتَابًا يَأْلَمُهُ مَنْشُورًا افْرًا كِتَابَكَ كَفَى بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ عَلَيْكَ حَسِيبًا

"Na kila mwanaadamu Tumemuambatanishia majaaliwa ya ‘amali zake shingoni mwake. Na Tutamtolea Siku ya Qiyaamah kitabu atakachokikuta kimekunjuliwa. [Ataambiwa]: "Soma kitabu chako! Nafsi yako inakutosheleza leo kukuhesabia dhidi yako."⁹⁶

Tunaamini Mizani itayowekwa siku ya Qiyaamah na hakuna yeote atayedhulumiwa:

فَمَنْ يَعْمَلْ مِنْقَالَ دَرَّةٍ حَيْرًا يَرَهُ وَمَنْ يَعْمَلْ مِنْقَالَ دَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ

"Basi yule atakayetenda kheri uzito wa chembe ya atomu basi ataiona. Na yule atakayetenda shari uzito wa chembe ya atomu basi ataiona."⁹⁷

فَمَنْ ثَقَلَثْ مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ وَمَنْ حَقَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ الَّذِينَ حَسِيبُوا أَنفُسَهُمْ فِي جَهَنَّمَ حَالِدُونَ تَلْفَعُ وُجُوهُهُمُ النَّارُ وَهُنْ فِيهَا كَالْجِلُونَ

"Basi yule ambaye mizani yake itakuwa nzito, hao ndio wenyewe kufaulu. Na yule ambaye mizani yake itakuwa khafifu, basi hao ni wale ambao zimekhasirika nafsi zao, [watakuwa] katika [Moto wa] *Jahannam* ni wenyewe kudumu. Moto utababua nyuso zao; nao humo [watakuwa] ni wenyewe nyuso zilizokunjana."⁹⁸

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهِ ۝ وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُبَرِّئُ إِلَّا مِثْلَهَا وَهُنْ لَا يُظْلَمُونَ

⁹⁵ 84:07-12

⁹⁶ 17:13-14

⁹⁷ 99:07-08

⁹⁸ 23:102-104

"Afanyae wema atalipwa mfano wake mara kumi. Na afanyae ubaya hatalipwa isipokuwa sawa nao tu na wao hawatadhuluiwa."⁹⁹

Tunaamini Uombezi mkubwa ambao itakuwa ni haki ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) peke yake. Baada ya Allaah kumpa idhini, atashufaia kwa Allaah ili viumbe wafanyiwe hesabu. Watakuwa na hali ngumu wasiyoiveza. Wataanza kwenda kwa Aadam, kisha Nuuh, kisha Ibraahiyim, kisha Muusa, kisha ‘Iysaa mpaka mwishoni waende kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam).

Tunaamini kuwepo uombezi kwa wale waumini walioingia Motoni watolewe. Uombezi huu ni kwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam), Mitume wengine, waumini na Malaika.

Vilevile tunaamini kuwa Allaah atawatoa watu kutoka Motoni kutokana na Fadhila na Huruma Wake pasi na uombezi wowote.

Tunaamini hodhi ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam). Maji yake ni meupe zaidi kuliko maziwa, matamu zaidi kuliko asali na yenyenye kunukia vizuri zaidi kuliko miski. Urefu wake na upana wake ni sawa na mwendo wa safari ya mwezi. Vikombe vyake ni vizuri sana na vingi kama nyota za mbinguni. Waumini katika Ummah wake ndio wataiendea. Atakayekunyuwa mara moja hatopata kiu tena baada ya hapo.

Tunaamini Njia ilioko juu ya Moto. Watu watapita juu yake kutegemea na matendo yao. Wa kwanza wao atapita kama umeme, wa pili atapita kama upepo, ndege au ngamia. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) atakuwa amesimama juu ya Njia na huku anasema:

"Ee Mola! Salimisha, salimisha."

⁹⁹ 06:160

Matendo ya waja yataisha na hapo ndipo watakuja baadhi hali ya kuwa wanatambaa. Kwenye ncha ya Njia kuna miba ilioamrishwa kumwangusha yule ilioamrishwa. Mwenye furaha ataokoka na mwangamivu atatumbukia Motoni.

Tunaamini yale yote yaliyotajwa katika Qur-aan na Sunnah kuhusiana na siku hii na hali zake - tunamuomba Allaah atusaidie kwazo.

Tunaamini uombezi wa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) kwa watu wa Peponi waingie. Uombezi huu ni maalum kwa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam).

Tunaamini Pepo na Moto. Pepo ni makazi ya starehe ambayo Allaah amewaandalia waumini wenyewe kumcha. Humo mna neema ambazo hakuna yejote ameshawahi kuziona, kuzisikia wala kujifikiria nazo.

فَلَا يَعْلَمُ نَفْسٌ مَا أَخْفِيَ لَهُمْ مِنْ فُرَّةٍ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

"Nafsi yoyote haijui yaliyofichiwa katika yanayoburudisha macho. Ni jazaa kwa yale waliyokuwa wakiyatenda."¹⁰⁰

Moto ni makazi ya adhabu ambayo Allaah (Ta’ala) amewaahidi makafiri madhalimu. Humo mna adhabu isiyoweza kufikiriwa.

إِنَّا أَعْنَدْنَا لِلظَّالِمِينَ نَارًا أَحَاطَ بِهِمْ سُرَادُقُهَا ۝ وَإِنْ يَسْتَغْشُوا يُعَذَّبُوا إِمَاءَ كَالْمُهْلِ يَشْوِي الْأُجُوْهُ ۝ يَقْسِنُ الشَّرَابُ وَسَاعَةٌ مُرْتَفَقًا

"Hakika Sisi Tumewaandalia madhalimu Moto ambao kuta zake zitawazunguka. Na wakiomba msaada watasaidiwa kwa [kupewa] maji kama mafuta meusi ya moto yanayobabua nyuso. Ubaya ulioje kinywaji hicho, na uovu ulioje mahali pa kupumzikia."¹⁰¹

Vinapatikana hivi sasa na havitotoweka hata siku moja.

¹⁰⁰ 32:17

¹⁰¹ 18:29

وَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَيَعْمَلْ صَالِحًا يُدْخَلْ جَنَّاتٍ بَحْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ حَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۖ قَدْ أَحْسَنَ اللَّهُ لَهُ رِزْقًا

“Na yeote [yule] anayemwamini Allaah na akatenda [’amali] njema, [basi Allaah] Atamuingiza mabustani yapitayo chini yake mito ni wenyе kudumu humo milele - Allaah Amekwishampa riziki nzuri.”¹⁰²

إِنَّ اللَّهَ لَعَنِ الْكَافِرِينَ وَأَعَدَ لَهُمْ سَعِيرًا حَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۖ لَا يَجِدُونَ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا يَوْمَ تُقْلَبُ فُخُوهُمْ فِي النَّارِ يَقُولُونَ يَا لَيْتَنَا أَطْعَنَا اللَّهُ وَأَطْعَنَا الرَّسُولَ

"Hakika Allaah Amewalaani makafiri na Amewaandalia [Moto wa] Sa'iyyraa. Ni wenyе kudumu humo milele. Hawatopata mlinzi na wala mwenye kunusuru. Siku zitakapopinduliwa nyuso zao Motoni, watasema: "Laiti tungelimitii Allaah na tungelimitii Mtume."¹⁰³

Tunashuhudia Pepo juu ya kila ambaye Qur-aan na Sunnah vimemtolea ushahidi, sawa ikiwa ni mtu kwa dhati yake au kwa maelezo. Waliopewa ushahidi kwa dhati zao ni pamoja na Abu Bakr, ‘Umar, ‘Uthmaan, ‘Aliy na wengine ambaa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) aliwateua kwa dhati zao. Mionganoni mwa zile sifa zilizotolewa ushahidi ni ushahidi wa imani ya muumini na uchaji Allaah wa mwenye kumcha.

Tunamshuhudia Moto kila ambaye Qur-aan na Sunnah vimemtolea ushahidi, sawa ikiwa ni mtu kwa dhati yake au kwa maelezo. Waliopewa ushahidi kwa dhati zao ni pamoja na Abu Lahab, ‘Amr bin Luhayy al-Khuzaa’iy na wengineo. Mionganoni mwa zile sifa zilizotolewa ushahidi ni ushahidi wa kufuru ya kafiri, shirki kubwa ya mshirikina na unafiki wa mnafiki.

Tunaamini fitina ya kaburi ikiwa na maana ya kwamba maiti ataulizwa kuhusu Mola, dini na Mtume Wake.

¹⁰² 65:11

¹⁰³ 33:64-66

يُبَشِّرُ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا بِالْقُوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ

"Allaah Huwathibitisha wale walioamini kwa kauli thabiti katika uhai wa dunia na Aakhirah."¹⁰⁴

Muumini atasema:

"Mola wangu ni Allaah, Uislamu ndio dini yangu na Muhammad ndio Mtume wangu."

Kuhusu kafiri na mnafiki watasema:

"Sijui. Niliwasikia watu wakisema kitu na mimi nikakisema."

Tunaamini kuwa waumini wataneemeshwa ndani ya makaburi:

الَّذِينَ تَنَوَّفَاهُمُ الْمَلَائِكَةُ طَيِّبُونَ ۝ يَقُولُونَ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ اذْهَلُوا اجْتَهَدُوكُنْتُمْ تَعْمَلُونَ

"Ambao Malaika huwafisha katika hali nzuri [Malaika] watasema: [kuwaambia Waumini]: "Salaamun 'Alaykum [amani iwe juu yenu]! Ingieni Peponi kwa yale mliyokuwa mkitenda."¹⁰⁵

Tunaamini kuwa madhalimu na makafiri wataadhibiwa ndani ya makaburi:

وَلَوْ تَرَى إِذَ الظَّالِمُونَ فِي غَمَرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلَائِكَةُ بَاسِطُو أَيْدِيهِمْ أَخْرِجُوا أَنْفُسَكُمْ ۝ الْيَوْمَ بُخْرُونَ عَذَابَ الْهُنُونِ إِنَّمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ عَلَى اللَّهِ غَيْرُ
الْحَقِّ وَكُنْتُمْ عَنْ آيَاتِهِ تَمْسَكُنُكُمْ

"Na lau ungeliona madhalimu pale wakiwa katika mateso makali ya mauti, na Malaika wamenyosha mikono yao [wakiwaambia]: "Zitoeni nafsi zenu! Leo mnalipwa adhabu ya kudhalilisha kwa yale mliyokuwa mkiyasema juu ya Allaah pasi na haki na kwa vile mliyyokuwa mkifanya kiburi juu ya Aayaat Zake."¹⁰⁶

¹⁰⁴ 14:27

¹⁰⁵ 16:32

¹⁰⁶ 06:93

Ahaadiyth kuhusiana na suala hili ni nyingi na zinajulikana. Ni lazima kwa muumini kuamini yale yote yaliyokuja katika Qur-aan na Sunnah juu ya mambo haya yenye kufichikana, pasi na kuyalinganisha na yale anayoyaona duniani. Mambo ya Aakhirah hayawezi kulinganishwa na mambo ya duniani, kwa sababu kuna tofauti kubwa kati ya hayo mawili.

Kuamini Qadar

Tunaamini Qadar, kheri na shari yake. Allaah amepanga makadirio ya viumbe kwa mujibu wa utanguliaji wa Ujuzi Wake na kutokana na vile Hekima Yake inavyopelekea.

Qadar ina ngazi nne:

1. Ujuzi. Tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) juu ya kila kitu ni Mjuzi. Kwa Elimu Yake ya milele na yenyewe kudumu anayajua yaliyokuwepo, yatayokuwepo na namna yatavyokuwepo. Katika Elimu Yake hakuna kitu kinachokuwa kipyaa baada ya kutokukijua na Elimu Yake haifikiwi na kitu kusahau.
2. Uandishi. Tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) ameandika kwenye Ubao uliohifadhiwa yatayokuwepo mpaka siku ya Qiyaamah:

أَنَّمَا تَعْلَمُ اللَّهُ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۝ إِنَّ ذَلِكَ فِي كِتَابٍ ۝ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

"Je, huelewi kwamba Allaah Anajua yale yote yaliyomo katika mbingu na ardhi? Hakika hayo yamo katika Kitabu. Hakika hayo kwa Allaah ni mepesi."¹⁰⁷

3. Utashi. Tunaamini kuwa kila kilichopo mbinguni na ardhini kinapitika kwa matakwa ya Allaah (Ta’ala). Hakukuwi kitu isipokuwa kwa Kutaka Kwake. Kile anachokitaka Allaah ndio huwa, na kile asichokitaka hakiwi.

4. Uumbaji. Tunaamini kuwa:

اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ ۝ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ لَّهُ مَقَالِيدُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ

"Allaah ni Muumbaji wa kila kitu, Naye juu ya kila kitu ni Mtegemewa. Pekee Anazo funguo za mbingu na ardhi."¹⁰⁸

¹⁰⁷ 22:70

Ngazi hizi nne zinawakilishwa na yale anayofanya Allaah (Ta’ala) na waja. Allaah anajua yale yote wanayoyasema waja, wanayoyafanya au kuyaacha. Anayaandika Kwake Mwenyewe (Ta’ala), Ameyataka na Kuyaumba:

لِمَن شَاءَ مِنْكُمْ أَن يَسْتَقِيمَ مَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

“Kwa yule atakaye miongoni mwenu anyooke [katika njia ya haki]. Na hamtotaka isipokuwa Atake Allaah Mola wa walimwengu.”¹⁰⁹

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا فَتَّلُوا وَلَكِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ

“Na lau Angelitaka Allaah wasingelipigana lakini Allaah Anafanya Ayatakayo.”¹¹⁰

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا فَعَلُوا فَلَدَرُهُمْ وَمَا يَفْتَرُونَ

“Na lau Allaah Angetaka wasingeliyafanya hayo. Basi waachilie mbali na [hayo] wanayoyatunga.”¹¹¹

وَاللَّهُ خَلَقُكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ

“Na hali Allaah Amekuumbeni na yale (yote) mnayoyafanya.”¹¹²

Lakini pamoja na hivyo, tunaamini kuwa Allaah (Ta’ala) amemjaalia mja kuwa na khiyari na uwezo wa kutenda.

¹⁰⁸ 39:62-63

¹⁰⁹ 81:28-29

¹¹⁰ 2:253

¹¹¹ 06:137

¹¹² 37:96

Dalili zifuatazo zinaonesha kuwa mja ana uhuru na uwezo wa kutenda:

1. Amesema (Ta’ala):

فَأُنْتُمْ حَرَثُكُمْ أَئِ شَتْنُمْ

"Basi ziendeeni konde zenu vyovyote mpendavyo."¹¹³

وَلَوْ أَرَادُوا لَهُ عِدَّةً
وَلَوْ أَرَادُوا الْخُرُوجَ لَأَعْدَّوْا لَهُ عِدَّةً

"Na lau wangelitaka kutoka [kwenda vitani], wanglediandaa maandalizi yake."¹¹⁴

Amethibitisha kuwa waja wanaweza kwenda kwa kutaka kwao na kufanya maandalizi kwa utashi wao.

2. Mja ameelekezwa maamrisho na makatazo. Lau asingekuwa na utashi wa khiyari na uwezo, basi angelikuwa ameelekezwa katika kitu asichoweza kukifanya. Ni kitu chenye kukataliwa na Hekima ya Allaah (Ta’ala), huruma Wake na maelezo Yake ya kweli:

لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا

"Allaah Hakalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya uwezo wake."¹¹⁵

3. Mwenye kufanya kitendo chema anasifiwa na mwenye kufanya kitendo kiovu analaumiwa. Kila mmoja analipwa kwa njia anayoistahiki. Lau ingelikuwa kitendo hakipitiki kwa utashi wa khiyari ya mja, kumsifu mwenye kufanya kitendo chema kungelikuwa hakuna maana yoyote na kumlaumu mwenye kufanya kitendo kiovu ingelikuwa ni dhuluma.

¹¹³ 02:223

¹¹⁴ 09:46

¹¹⁵ 02:286

4. Allaah amewatuma Mitume:

رُسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونُ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ

"Mitume ni wabashiriaji na waonyaji ili pasikuweko kutoka kwa watu hoja yoyote juu ya Allaah baada ya [kuletwa] Mitume."¹¹⁶

Lau mja angelikuwa ni mwenye kutenda pasi na kupenda na kutaka kwake, hoja yake ingelikuwa si yenyekubatilika baada ya kutumwa Mitume.

5. Kila mwenye kutenda au kukiacha kitu, anahisi kuwa amekifanya bila ya kutenzwa nguvu. Anasimama, anakaa, anaingia, anatoka na anasafiri kwa kutaka kwake. Hahisi kabisa kuwa kuna yejote mwenye kumlazimisha kufanya hayo. Anatofautisha wazi wazi baina ya anapofanya kitu kwa khiyari yake na pindi anapolazimishwa. Hali kadhalika Shari’ah imetofautisha kati ya hayo mawili kwa njia ya busara. Mlazimishwaji haadhibiwi kwa kitu alichotenzwa nguvu, ikiwa kitendo hicho kinahusiana na haki ya Allaah (Ta’ala).

Tunaona kuwa mtenda dhambi hana hoja yoyote kwa dhambi yake kutokana na Qadar ya Allaah (Ta’ala). Mtenda dhambi anafanya dhambi kwa khiyari yake bila ya kujua kuwa Allaah (Ta’ala) amemkadiria nayo, kwa sababu hakuna yejote anayejua makadirio ya Allaah (Ta’ala) isipokuwa baada ya kutokea kilichopangwa:

وَمَا تَدْرِي نَفْسٌ مَّا ذَا تَكْسِبُ غَدَارًا

"Na nafsi yoyote haijui nini itachuma kesho."¹¹⁷

Vipi basi itakuwa ni sahihi kwa mtu huyu kutumia hoja kitu ambacho yeje mwenyewe hajui kinapeleke katika nini? Allaah (Ta’ala) amebatilisha hoja hii kwa Kauli Yake:

¹¹⁶ 04:165

¹¹⁷ 31:34

سَيَقُولُ الَّذِينَ أَشْرَكُوا لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا أَشْرَكْنَا وَلَا آبَاؤُنَا وَلَا حَرَمَنَا مِنْ شَيْءٍ ۖ كَذَلِكَ كَذَبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ حَتَّىٰ ذَأْفُوا بِأَسْنَانٍ ۗ فَلَمْ يَلْعَمْهُمْ إِنْ عَلِمْتُمْ ۖ إِنْ تَتَّخِذُ جُوهُرًا لَّنَا ۖ إِنْ تَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّرَفُ وَإِنْ أَنْتُمْ إِلَّا تَخْرُصُونَ

"Watasema wale walioshirikisha: "Lau Allaah Angetaka tusingelifanya shirki, wala baba zetu [wasingelishirikisha pia] na wala tusingelihamlisha chochote." Hivyo ndivyo walivyokadhibisha wale wa kabla yao mpaka walipoonja adhabu Yetu. Sema: "Je, mna elimu yoyote mtutolee? Hamfuati isipokuwa dhana tu, nanyi si lolote ila mnabuni uongo."¹¹⁸

Tunamwambia mtenda dhambi ambaye anailaumu Qadar yafuatayo:

Kwa nini hukufanya kitendo chema kwa kukadiria ya kwamba Allaah (Ta’ala) amekupangia nacho? Hakuna tofauti kati yacho na kati ya dhambi inayofanywa kwa kutokujua yaliyopangwa kabla ya kutokea kwake.

Kutokana na sababu hiyo wakati Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) alipowaambia Maswahabah ya kwamba kila mmoja ameshaandikiwa mahali pake Peponi au Motoni. Wakasema: "Situache kutenda na tutegemee hayo?" Akajibu: "**Hapana, tendeni, hakika kila mmoja amesahilishiwa kwa yale aliyouumbiwa kwayo.**"

Tunamwambia mtenda dhambi ambaye anailaumu Qadar yafuatayo:

Hebu tuchukulie unataka kusafiri kwenda Makkah na uko na njia mbili. Mtu mwaminifu akakueleza kuwa njia moja ni ya khatari na ngumu, na njia nyingine ni ya usalama na nyepesi. Hapa utachukua hii ya pili. Ni jambo lisilowezekana ukachukua ile ya kwanza na kusema: "Imeshakadiriwa kwangu." Lau utafanya hivo, watu watachukulia kuwa ni mwendawazimu.

Tunasema pia:

Tuseme kuwa umepewa kazi mbili. Moja katika kazi hizo ina mshahara mnono. Vipi basi utaweza kuchagua kazi ilio na mshara wa chini halafu uilaumu Qadar?

¹¹⁸ 06:148

Tunasema kumwambia tena:

Tuchukulie kuwa umesibiwa na maradhi ya kimwili. Unabisha hodi mlango wa kila daktari ili kujitibisha. Unavumilia maumivu baada ya upasuaji na madawa machungu. Ni kwa nini basi usifanye vivyo hivyo kwa moyo wako ulio mgonjwa kwa madhambi?

Tunaamini kuwa shari hainasibishwi kwa Allaah (Ta’ala) kutokana na ukamilifu wa Huruma na Hekima Yake. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema:

"Shari haitoki Kwako."

Ameipokea Muslim.

Maamuzi ya Allaah (Ta’ala) yenewe sio shari, kwa sababu yametokamana na huruma na hekima. Hata hivyo shari inaweza kuwa katika yale yaliyoamuliwa. Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa sallam) amesema kwenye du’aa ya Qunuut aliyoamfunza al-Hasan:

"Nilinde na shari Uliyoamua."

Amefungamanisha shari na yale Aliyoyaamua. Pamoja na hivyo, shari katika yaliyopangwa sio shari ilio safi na ilio tupu. Bali ni shari kwa mtazamo fulani na ni kheri kwa mtazamo mwingine. Ufisadi unaotokea katika ardhi wa ukame, maradhi, ufakiri na khofu ni shari, lakini vilevile ni kheri kwa mtazamo mwingine. Allaah (Ta’ala) amesema:

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ إِمَّا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ لِيُنْدِقُهُمْ بَعْضُ الَّذِي عَمِلُوا لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ

"Ufisadi umedhihiri katika nchi kavu na baharini kwa sababu ya yale iliyochuma mikono ya watu ili Awaonjeshe baadhi ya ambayo wameyatenda ili wapate kurejea [kutubu]."¹¹⁹

¹¹⁹ 30:41

Kukata mkono wa mwizi na kumpiga mawe mzini fu ni shari kwa nisba ya mtendaji, lakini ni kheri kwao kwa kuzingatia ya kwamba madhambi yao yanasehewa. Hawatoadhibiwa duniani na Aakhirah. Hali kadhalika ni kheri kwa sababu kuna kuhifadhiwa kwa mali, heshima na ukoo.

Matunda ya ‘Aqiydah hii

‘Aqiydah hii ya kimbingu, ilio na misingi hii mikubwa, inampa mwenye nayo matunda mengi mazuri.

Kumuamini Allaah (Ta’ala) na Majina na Sifa Zake, kunamfanya mja kumpenda Allaah na kumuadhimisha. Kunampelekea yeye kutekeleza maamrisho Yake na kuijepusha na makatazo Yake. Kwa hayo kunapatikana kwa mtu binafsi na jamii furaha kamilifu duniani na Aakhirah.

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَى وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيهِ حَيَاةً طَيِّبَةً ۖ وَلَئِنْجَرِيَّتُهُمْ أَجْرُهُمْ بِأَخْسَى مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

"Mwenye kutenda mazuri mionganini mwa wanamume au wanawake naye ni Muumin, Tutamhuisha uhai mzuri, na bila shaka Tutawalipa ujira wao kwa mazuri zaidi ya yale waliyokuwa wakitenda."¹²⁰

Matunda yanayopatikana kwa kuwaamini Malaika, ni pamoja na yafuatayo:

1. Ujuzi juu ya Ukubwa wa Muumbaji Wao (Tabarak wa Ta’ala), Uwezo Wake na Nguvu Zake.
2. Kumshukuru (Ta’ala) kwa kuwajali waja Wake. Amewawakilisha Malaika hawa kuwahifadhi, kuandika matendo yao na maslahi yao mengine.
3. Kuwapenda Malaika kutokana na ‘ibaadah wanazomfanyia Allaah (Ta’ala) kwa njia timilifu na kuwaombea kwao msamaha waumini.

Miongoni mwa matunda yanayopatikana kwa kuamini Vitabu, ni pamoja na yafuatayo:

1. Ujuzi wa kumjua Allaah (Ta’ala) na namna anavyowajali waja Wake kwa vile ameteremsha Kitabu kwa kila Ummah ambacho anawaongoza kwacho.

¹²⁰ 16:97

2. Dalili ya Hekima ya Allaah (Ta’ala) pale ambapo ameweke katika Vitabu hivi kwa kila Ummah yale yenye kuendana na wao. Kitabu cha mwisho katika Vitabu hivi ni Qur-aan Kubwa na inaendana na viumbe wote katika kila zama na mahala mpaka siku ya Qiyaamah.

3. Kushukuru neema ya Allaah (Ta’ala) juu ya hilo.

Miongoni mwa matunda yanayopatikana kwa kuamini Mitume, ni pamoja na yafuatayo:

1. Ujuzi wa kujua Huruma wa Allaah (Ta’ala) na kuwa anawajali viumbe Wake kwa kuwatumia Mitume watukufu kwa ajili ya uongofu na maelekezo.

2. Kumshukuru Allaah (Ta’ala) kwa neema hii kubwa.

3. Kuwapenda Mitume, kuwaadhimisha na kuwasifu kwa njia inayotakikana. Pamoja na yote wao ni Mitume wa Allaah (Ta’ala) na waja wasafi. Wamemuabudu Allaah, kufikisha ujumbe Wake, kuwanasihi waja Wake na kuvumilia maudhi yao.

Miongoni mwa matunda yanayopatikana kwa kuamini siku ya Mwisho, ni pamoja na yafuatayo:

1. Kupuria kumtii Allaah (Ta’ala) kwa malengo ya kulipwa siku hiyo na kuijepusha na kumuasi kwa kukhofia kuadhibiwa siku hiyo.

2. Muumini kuliwazika na furaha na vipumbazo vyta duniani vinavyompita kutokana na neema na malipo ya Aakhirah anayoyatarajia.

Miongoni mwa matunda yanayopatikana kwa kuamini Qadar, ni pamoja na yafuatayo:

1. Kumtegemea Allaah (Ta’ala) pindi kunapotokea jambo, kwa kuwa sababu na chenye kusababishwa yote mawili yanatokamana na mipango na makadirio ya Allaah (Ta’ala).

2. Nafsi yenyе raha na utulivu wa moyo. Pindi mtu anapojuwa kuwa mambo yote yanatokamana na aliyoyapanga Allaah (Ta’ala) na kuwa yanayochukiwa ni lazima yapitike, nafsi inapata starehe na moyo unapata utulivu na kuridhia maamuzi ya Mola. Hakuna mwenye maisha mazuri kabisa, moyo wenyе raha na utulivu mkubwa kabisa kama yule mwenye kuamini Qadar.

3. Mtu asijione pindi anapopata kitu maalum, kwa sababu kupata kitu hicho kunatokamana na neema ya Allaah. Hivyo amshukuru Allaah na aache majivuno.

4. Mtu kutokuwa na wasiwasi na kuhuzunika pindi anapokosa kitu maalum au kufikwa na kitu chenye kuudhi. Yote hayo yanatokamana na mipango ya Allaah (Ta’ala), Mola wa mbingu na ardhi. Yaliyopangwa ni lazima yapitike na hakuna namna ya kuyazuia. Kwa ajili hiyo awe na subira juu ya hilo na atarajie malipo. Haya ndio anayoashiria Allaah (Ta’ala) pale anaposema:

مَا أَصَابَ مِنْ مُّصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ أَنْ تَبَرَّأُهَا ۝ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ بِسِيرٍ لِكُلِّ أَنْوَافِهِ تَأْسُوا عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ وَلَا تَفْرُجُوا
بِمَا آتَكُمْ ۝ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَقُحُورٍ

“Hakuna msiba wowote unaokusibuni katika ardhi au katika nafsi zenu isipokuwa umo katika Kitabu kabla Hatujauumba [huo msiba] - hakika hayo kwa Allaah ni mepesi. Ili msisononeke juu ya yale yaliyokuondokeeni na wala msifurahie kwa yale Aliyokupeni; na Allaah Hapendi kila mwenye kujinata, anayejifakharisha.”¹²¹

Tunamuomba Allaah (Ta’ala) atuthibitishe katika ‘Aqiydah hii, atutunukie matunda yake, atuzidishe katika fadhila Zake, asizipotoshe nyoyo zetu baada ya kuziongoza na aturehemu - hakika Yeye ndiye mwenye kutoa - himdi zote ni Zake Allaah, Mola wa walimwengu.

Swalah na salaam zimwendee Mtume wetu Muhammad, familia yake, Maswahabah zake na wenyе kuwafuata kwa wema.

¹²¹ 57:22-23

Imeandikwa na:

Muhammad bin Swaalih bin ‘Uthaymiyn

Tarehe. 30 Shawwaal 1404 H